**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# MWONGOZO WA UTOAJI CHANJO DHIDI YA MAGONJWA YA MIFUGO KWA MFUMO WA USHIRIKIANO KATI YA SEKTA YA UMMA NA BINAFSI






***TOLEO LA KWANZA 2021***

**YALIYOMO**

**Dibaji** .......... 3
**1.0 UTANGULIZI** .......... 4
**2.0 MALENGO YA MWONGOZO HUU** .......... 4
**3.0 UMUHIMU WA CHANJO KWA MIFUGO.** .......... 5
**4.0 MAMBO YA KUZINGATIA ILI KUPATA UFANISI KATIKA UTOAJI WA CHANJO** .......... 5
**5.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KABLA YA KUTOA CHANJO** .......... 6
5.1 Magonjwa ya kipaumbele yanayohusika na Mwongozo huu .......... 6
5.2 Ushirikishwaji wa wadau katika maandalizi na utekelezaji wa utoaji wa chanjo .......... 6
5.3 Bei Elekezi ya chanjo za magonjwa ya kipaumbele .......... 6
**6.0 SERA SHERIA NA MIONGOZO INAYOSIMAMIA UTOAJI WA CHANJO ZA WANYAMA** .......... 7
**7.0 MAJUKUMU YA WADAU** .......... 8
7.1 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi .......... 8
7.2 Majukumu ya TAMISEMI .......... 9
7.3 Majukumu ya Ofisi za Mikoa (Regional Secretariat) .......... 9
7.4 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa .......... 10
7.5 Majukumu ya Watoa Huduma Binafsi .......... 11
7.6 Majukumu ya Serikali ya Kijiji au Mtaa .......... 11
7.7 Majukumu ya mfugaji .......... 12
**8. UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU** .......... 12

## Dibaji

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakabiliana na changamoto za magonjwa ya mifugo yanayoathiri afya ya wanyama, binadamu na biashara kwa kuzingatia matakwa ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006, Sheria ya Magonjwa ya Wanyama ya Mwaka 2003, Sheria ya Ustawi wa Wanyama na Kanuni mbalimbali za Mifugo. Utoaji wa chanjo ni njia rahisi ya kutegemewa na yenye gharama nafuu katika kudhibiti magonjwa mengi ya mifugo.

Wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Umma, watoa huduma katika Sekta ya Umma na Binafsi wanayo majukumu yanayotegemeana, na yakifanyika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo, lengo kuu la utoaji wa chanjo litafikiwa.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitengeneza Kanuni za Chanjo na Uchanjaji za Mwaka 2020 zinazosimamia suala zima la chanjo za wanyama nchini. Vilevile, imetengeneza Mwongozo wa Utoaji wa Chanjo dhidi ya Magonjwa ya Mifugo kwa mfumo wa ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi wa mwaka 2021. Mwongozo huu unaainisha mahitaji, majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali katika zoezi la utoaji wa chanjo kwa wanyama ili kufikia lengo la jumla la kulinda afya ya wanyama, binadamu na kukuza soko la mifugo na mazao yake. Wadau walioainishwa kwenye mwongozo ni pamoja na: Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretariate za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, watoa huduma wa Sekta Binafsi, Serikali za vijiji na Wafugaji.

Mwongozo unaainisha ushiriki na vigezo vya watoa huduma, usimamizi na upimaji wa ufanisi wa zoezi la chanjo na namna ya kuhakisha kuwa mifugo inapata huduma ya chanjo kwa kutumia chanjo zenye ubora na kwa wakati sahihi kutoka kwa watoa huduma waliokidhi vigezo wa Sekta ya Umma na Binafsi kwa gharama nafuu. Aidha, utekelezaji wa Mwongozo huu utachangia kuboresha huduma ya utoaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya wanyama na kuongeza tija ya uzalishaji na biashara katika Sekta ya mifugo kwa ujumla.

Mwongozo huu umetolewa na Idara ya Huduma za Mifugo na utaanza kutumika mwezi Januari, 2021.

Prof. Hezron E. Nonga
**Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo**
**20 Januari 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Tanzania ni moja ya nchi barani Afrika yenye mifugo mingi na hivyo kufanya sekta ya mifugo kuwa na umuhimu mkubwa katika uchumi wa kaya na kuwa na uwezo wa kuchangia sana katika pato la Taifa. Kwa sasa, sekta hii huchangia kiasi cha asilimia 7.6. Mchango huu unaweza kuongezeka iwapo mipango madhubuti itachukuliwa kama inavyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo, 2006 na programmu ya Maendeleo ya Mifugo. Mpaka sasa, Tanzania ina jumla ya ng'ombe milioni 33.4; mbuzi 21.29 milioni; kondoo 5.65 milioni; nguruwe 2.14 milioni; punda wapatao 657,389; kuku wa kiasili ni milioni 38.77; na wa kisasa ni milioni 44.51.

Kama ilivyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo, 2006, moja ya changamoto kubwa inayokabili sekta hii ni uwepo wa athari kubwa za magonjwa mbalimbali ya mifugo. Magonjwa ya mifugo sio tu yanapunguza uzalishaji bali pia yanaathiri biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi na kudumaza, kwa kiasi kikubwa, mchango wa sekta ya mifugo katika kuchangia pato la kaya kwa wafugaji na taifa kwa ujumla. Aidha, baadhi ya magonjwa ya wanyama huambukiza binadamu (zoonosis). Hivyo, uwepo wa maambukizi ya magonjwa katika ya mifugo, wanyamapori na binadamu ni suala ambalo linalazimisha uwepo wa mikakati endelevu na shirikishi ya kudhibiti wa magonjwa husika.

Udhibiti wa magonjwa ya wanyama unafanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo utoaji wa matibabu, utoaji wa chanjo kwa magonjwa ya kipaumbele; kuogesha wanyama kwa kutumia dawa za kuua kupe na wadudu wengine; kuweka karantini na mamlaka husika kwa magonjwa muhimu ya kupaumbele wakati milipuko inapotokea na kuwekwa kwa mikakakti ya kuzuia mwingiliano wa kundi moja la mifugo na kundi jingine. Kwa ujumla, utoaji wa chanjo ni njia rahisi, ya kutegemewa na yenye gharama nafuu katika kuzuia magonjwa. Mwongozo huu unajikita katika utoaji wa chanjo za wanyama kwa kushirikisha wadau katika ngazi mbalimbali.

## 2.0 MALENGO YA MWONGOZO HUU

### 2.1 Lengo kuu la mwongozo

Mwongozo unalenga kuainisha mahitaji, majukumu na wajibu ya wadau mbalimbali katika zoezi la utoaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya wanyama, ili kufikia lengo la jumla la kulinda afya ya wanyama, binadamu na kukuza soko la ndani na nje ya nchi.

### 2.2 Malengo mengine ya mwongozo

(a) Kuainisha majukumu ya kila mdau katika kudhibiti wa magonjwa ya wanyama kwa kutumia chanjo;

(b) Kuhakikisha ushiriki wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma unafanyika kwa kuzingati Sheria, Kanuni na Miongozo kwa faida ya wadau wote;

(c) Kuhakikisha kuwa mfugaji anapatiwa chanjo yenye ubora kwa kutumia wataalamu waliothibitishwa na wanaosimamiwa na mamlaka zinazotambulika kisheria;

(d) Kuhakikisha kuwa utoaji wa chanjo unaambatana na ufuatiliaji wa ufanisi wa zoezi zima la chanjo.

## 3.0 UMUHIMU WA CHANJO KWA MIFUGO

Umuhimu wa chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo ni pamoja na:

(a) Kuwa njia ya uhakika ya kulinda afya ya wanyama;

(b) Kudhibiti magonjwa yasiyoweza kutibika hususan yanayotokea kwa njia ya mlipuko;

(c) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo yaliyo bora na salama;

(d) Kuongeza kuzaliana kwa mifugo na kukua haraka;

(e) Kuepuka hasara inayotokana na kutibu mifugo iliyougua na inayokufa;

(f) Kuwa na mifugo yenye ubora ambayo itapata soko na bei nzuri ndani na nje ya nchi;

(g) Kupata malighafi bora za viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo;

(h) Kuepuka magonjwa yanayoambukiza kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na;

(i) Kupunguza uwezekano wa kuongezeka kwa usugu wa vimelea dhidi ya dawa zinazotumika katika matibabu.

## 4.0 MAMBO YA KUZINGATIA ILI KUPATA UFANISI KATIKA UTOAJI WA CHANJO

Pamoja na faida ya chanjo, ufanisi katika utoaji wa chanjo unategemeana na:

(a) Kuwa na chanjo yenye ubora inayoweza kutoa kinga madhubuti kwa mnyama anayechanjwa;

(b) Kuwa na mnyonyoro wa ubaridi unaotunza ubora wa chanjo husika hadi inapotumika kwa mnyama;

(c) Weledi wa wataaalamu na kuzingatia miiko katika utoaji wa chanjo;

(d) Kalenda ya utoaji chanjo inayozingatia uwepo wa magonjwa na uwezekano wa maambukizi;

(e) Kuchanja wanyama wote wanaostahili kuchanjwa kwenye eneo husika;

(f) Uwepo wa elimu ya kutosha kwa wadau/wafugaji juu ya hasara za magonjwa na faida ya chanjo na;

(g) Mfumo imara wa usimamizi, ufuatiliaji na udhibiti wa zoezi la chanjo.

## 5.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KABLA YA KUTOA CHANJO

### 5.1 Magonjwa ya kipaumbele yanayohusika na Mwongozo huu

Kwa kuzingatia athari za magonjwa ya wanyama na magonjwa yanayoenezwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu ifuatayo ni orodha ya magonjwa ya kipaumbele ambayo yote hudhibitiwa kwa njia ya chanjo:

(a) Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP);
(b) Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP);
(c) Sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR);
(d) Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD);
(e) Ugonjwa wa Kimeta (Anthrax);
(f) Ugonjwa wa Kutupa Mimba (Brucellosis);
(g) Ugonjwa wa Mapele Ngozi (LSD);
(h) Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (RVF);
(i) Ugonjwa wa Ndigana Kali (ECF);
(j) Ugonjwa wa Mdondo kwa kuku (ND);
(k) Ugonjwa wa Marek's kwa kuku;
(l) Ugonjwa wa Gumboro kwa kuku;
(m) Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa (Rabies).

### 5.2 Ushirikishwaji wa wadau katika maandalizi na utekelezaji wa utoaji wa chanjo

Wadau wa utoaji na upokeaji wa huduma ya chanjo wanahitaji kushirikishwa katika maandalizi ili kuwa na uelewa wa pamoja wa umuhimu na kila kinachotegemewa kutokea kutokana na zoezi zima la chanjo. Wafugaji kupitia Chama Cha Wafugaji Tanzania (CCWT) wanahitaji kufahamishwa juu ya malengo ya zoezi husika, kiwango kinachategemewa kufikiwa, chanjo inayotumika na namna watakavyoshiriki ikiwa ni pamoja na kuchangia gharama za chanjo husika.

### 5.3 Bei Elekezi ya chanjo za magonjwa ya kipaumbele

Kufuatia Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003 kifungu cha 3 kifungu kidogo 2g na Kanuni za Chanjo na Uchanjaji (The Animal Vaccine and Vaccination Regulations) za Mwaka 2020 ambazo ni Kanuni Na.180 kifungu cha 14B pamoja na C zikisomwa kwa pamoja; bei elekezi ya chanjo za magonjwa 13 ya kipaumbele ilitangazwa rasmi tarehe 13/05/2020 na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania **(Jedwali Na.1)**.

**JEDWALI NA.1: MAGONJWA 13 YA KIPAUMBELE NA BEI ELEKEZI ZA CHANJO ZA MIFUGO**

**A. CHANJO ZINAZOZALISHWA NA WAKALA WA MAABARA TANZANIA – TVLA**

| S/N | Ugonjwa | Bei ya dukani kwa dozi 1 (shs) | Bei ya kuchanjia kwa dozi 1 (shs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) | 300 | 550 |
| 2. | Chambavu (Black Quarter) | 500 | 800 |
| 3. | Kimeta (Anthrax) | 300 | 500 |
| 4. | Chambavu & Anthrax (Tecoblax ) – Ng'ombe | 560 | 800 |
| | Chambavu & Kimeta (Tecoblax ) – Mbuzi & Kondoo | 280 | 500 |
| 5. | Kutupa Mimba (Brucellosis) | 1,000 | 1,500 |
| 6. | Mdondo kwa kuku (Newcastle disease) | 50 | 50 |
| **B. CHANJO ZINAZOZALISHWA NJE YA NCHI** | | | |
| 7. | Mapele Ngozi (Lumpy Skin Disease) | 400 | 600 |
| 8. | Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) | 200 | 350 |
| 9. | Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP) | 200 | 350 |
| 10. | Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) | 2,500 | 3,000 |
| 11. | Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa (Rabies) | 1,500 | 1,500 |
| 12. | Ndigana Kali (ECF) | 10,000 | 17,000 |
| 13. | Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley Fever) | 400 | 700 |

Bei hizi zitatumika Tanzania Bara pekee zinaweza kubadilika kulingana na upatikanaji wa chanjo. Aidha, zitakuwa zikipitiwa na kuhuishwa na kamati ya ushauri ya chanjo iliyoundwa chini ya Kanuni za Chanjo na Uchanjaji za Mwaka 2020 ili kumshauri Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo.

## 6.0 SERA, SHERIA NA MIONGOZO INAYOSIMAMIA UTOAJI WA CHANJO ZA WANYAMA

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006; Sera ya Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binfasi ya 2009 (National Public-Private Partnership, 2009), Waraka wa Rais Namba 1 wa Mwaka 2002; Hotuba ya Rais ya mwezi Novemba 2020 wakati anazindua Bunge la 12 na Ilani ya CCM 2020-2025 zimetoa mwelekeo kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kutoa huduma za afya ya mifugo ikiwemo utoaji wa chanjo. Pia, utoaji wa huduma ya chanjo kwa kutumia Sekta ya Umma na Sekta Binafsi unasimamiwa na Sheria Na. 17 ya Magonjwa ya Wanyama (The Animal Disease Act) ya Mwaka 2003, na Sheria Na. 16 ya Veterinari (Veterinary Act) ya Mwaka 2003 ambazo kwa pamoja

zinasimamia udhibiti wa magonjwa na watoa huduma za mifugo nchini. Pia, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na 19 ya mwaka 2008 na Marekebisho yake ya Mwaka 2010, inasimamia haki za na ustawi wa wanyama, ikiwemo kukingwa dhidi ya magonjwa vilevile ina mchango wake katika mifumo ya utoaji huduma ya afya ya wanyama. Aidha, Kanuni za Chanjo na Uchanjaji za Mwaka 2020 zinazosimamia chanjo na uchanjaji zinatambua na kuainisha majukumu na mipaka ya wataalamu wa Sekta Binafsi na Sekta Umma na wadau wengine wa pemebejeo, wafugaji katika utoaji na ushiriki kwenye zoezi la chanjo.

Hivyo, kwa kuzingatia Sera za kitaifa, Sheria na Kanuni tajwa hapo juu; na maelekezo mbalimbali ya kitaifa, mwongozo huu unatoa utaratibu wa utoaji wa huduma ya chanjo (Uchanjaji) kwa kutumia ushirikishwaji wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Lengo ni kuwa na utaratibu mzuri unaotoa majukumu na wajibu wa kila mdau katika kutoa huduma ya chanjo za wanyama nchini. Aidha, mwongozo umeainisha wadau husika ambao ni:

(a) Wizara ya Mifugo na Uvuvi,
(b) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)
(c) Ofisi za Mikoa;
(d) Mamlaka za Serikali za Mitaa,
(e) Wazalisha, waagizaji na wasambazaji wa chanjo nchini;
(f) Watoa huduma ya chanjo kutoka Sekta Binafsi,
(g) Serikali za vijiji au mitaa na;
(h) Wafugaji na wamiliki wa mifugo wenyewe na vyama vyao.

## 7.0 MAJUKUMU YA WADAU

### 7.1 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi

(a) Kutunga Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati kuhusu kudhibiti magonjwa kwa njia ya chanjo na kusimamia utekelezaji wake;
(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kujua mahitaji na upatikanaji wa chanjo za wanyama zenye ubora nchini na vitendea kazi vya uchanjaji;
(c) Kuweka bei elekezi za chanjo kwa njia shirikishi zitakazolipwa na wafugaji;
(d) Kubainisha sifa na kusajili watoa huduma za chanjo (umma na binafsi);
(e) Kuainisha na kusajili makampuni ya uagizaji au uzalishaji wa chanjo za wanyama;
(f) Kuweka utaratibu endelevu wa makampuni ya uzalishaji au uagizaji kupata, kuhifadhi na kusambaza chanjo katika ubora unaohitajika;
(g) Kuandaa ratiba za chanjo katika maeneo husika na nchi nzima kwa ujumla kulingana na epidemiolojia ya magonjwa yaliyopo na yanayoibuka;
(h) Kuratibu zoezi la utoaji chanjo ikishirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine;
(i) Kuandaa taratibu (Protocol) za utoaji chanjo kwa kila aina ya chanjo;

(j) Kutoa elimu ya afya ya mifugo na umuhimu wa chanjo kwa wafugaji na kwa umma kwa kushirikiana OR-TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika;
(k) Kuchukua sampuli na kupima ubora (effectiveness) wa uchanjaji, utengenezaji na usambazaji chanjo;
(l) Kutathimini ufanisi wa chanjo na zoezi la chanjo kwa kushirikiana na wadau wengine;
(m) Kuandaa na kusambaza nakala laini ya daftari la kumbukumbu za chanjo kwa ajili ya wafugaji;
(n) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza au kusimamia zoezi la chanjo kwa kuzingatia Sheria;
(o) Kuweka utaratibu wa kuzindua mazoezi ya chanjo kitaifa na kikanda pale inapowezekana;
(p) Kuhakisha Waraka wa Rais wa 2002 wa kutenga asilimia 15 ya maduhuli yanayotokana na mifugo unawekwa kisheria ili kuweza kuchangia katika zoezi zima la uchanjaji wa mifugo;
(q) Kuweka taratibu zitakazotumika katika kuhakikisha kuwa wataalamu wanaohusika katika utoaji chanjo ni wale wanaokidhi vigezo;
(r) Kushirikiana na OR-TAMISEMI katika kuratibu, kufuatilia na kufanya tathimini za utoaji chanjo na;
(s) Kushirikiana na chama cha wafugaji na wadau wengine katika kupanga na kuwezesha zoezi la chanjo ikiwemo utoaji wa bei elekezi na uhamasishaji.

## 7.2 Majukumu ya TAMISEMI

(a) Kuwa kiungo kati ya Wizara na Tawala za Mikoa katika kufanikisha utekelezaji wa maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu utoaji wa huduma za chanjo kwa wafugaji;
(b) Kusimamia Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali zinazohusiana na utoaji wa chanjo;
(c) Kutoa mwongozo na ushauri kwa Mikoa katika mambo ya kisheria na utaratibu kuhusiana na utoaji wa chanjo;
(d) Kujenga mazingira mazuri katika kuimarisha huduma za kijamii na kiuchumi katika Mikoa, ikiwa ni pamoja na suala la utoaji chanjo;
(e) Kuratibu, kushauri, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa zoezi la utoaji wa chanjo na;
(f) Kufuatilia na kukagua utendaji wa mamlaka za Mikoa, Serikali za Mitaa katika utoaji wa chanjo.

## 7.3 Majukumu ya Ofisi za Mikoa (Regional Secretariat)

(a) Kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa kuhakikisha utekelezaji wa mazoezi ya chanjo kwa pamoja ndani ya mkoa husika;
(b) Kuhamasisha zoezi la utoaji wa chanjo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(c) Kutoa usaidizi wa kitaalam (Technical backstopping) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(d) Kuwa kiungo kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, OR-TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika usimamizi utekelezaji na ufuatiliaji wa kampeni za chanjo na;

(e) Kuweka kanzidata ya watoa huduma binafsi waliopo Mkoani na uwezo wao katika raslimali watu na rasilimali fedha.

### 7.4 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

(a) Kuhakikisha mifugo yote inapata chanjo kwenye Halmashauri husika kulingana na kalenda ya chanjo;

(b) Kuwasiliana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu mipango na taratibu za mazoezi ya chanjo;

(c) Kuratibu na kutekeleza zoezi la chanjo kwa kushirikisha watoa huduma binafsi na wataalamu walioko katika Halmashauri katika kuleta ufanisi na kuzingatia ratiba za uchanjaji kama zilivyopendekezwa na Wizara. Halmashauri zinaweza kufanya marekebisho ya ratiba za uchanjaji kulingana na mazingira halisi yaliyopo. Katika kufanikisha zoezi la utoaji wa chanjo, Daktari wa Mifugo wa Wilaya ndiye atakayekuwa msimamizi wa zoezi zima la utoaji chanjo kwenye Halmashauri;

(d) Kuteua na kuweka mikataba na wazabuni wa Sekta Binafsi waliosajiliwa na Baraza la Veterinari Tanzania kutoa huduma ya chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo pale ambapo Halmashauri itaona inafaa;

(e) Kuhamasisha na kuwaelimisha wafugaji na wadau wengine kuhusu umuhimu wa kila mfugaji kuchanja mifugo kwa gharama ya mfugaji mwenyewe;

(f) Kushirikisha wafugaji, Vyama vya Wafugaji na Serikali za Vijiji au Mitaa katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa zoezi la kutoa chanjo;

(g) Kuhakikisha uwepo wa rasilimali zote muhimu katika zoezi la chanjo ikiwa ni pamoja na usafiri na vifaa vingine vya chanjo kama vile majokofu, vibebea chanjo, mabomba ya sindano na sindano kabla ya kuruhusu zoezi la chanjo kuanzishwa. Ushirikishwaji wa Makampuni husika ya usambazaji wa chanjo na watoa huduma katika suala hili ni muhimu;

(h) Kuandaa maeneo ya kuhifadhi chanjo na kuhakikisha kuwepo kwa mnyororo baridi wakati wote;

(i) Kuandaa kishirikishi miundombinu inayotakiwa ya kutoa chanjo kwa mifugo;

(j) Kuweka utaratibu wa kutambua mifugo iliyopata chanjo ili kurahisisha ufuatiliaji mifugo isiyochanjwa;

(k) Kudurufu na kusambaza daftari la kumbukumbu za chanjo kwa kila mfugaji;

(l) Kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kutathimini ufanisi wa chanjo na uchanjaji wakati na baada ya zoezi la chanjo;

(m) Kufuatilia kwa karibu matumizi sahihi ya chanjo kwa wafugaji na kuhakikisha chanjo zinabaki na ubora wake muda wote;
(n) Kuhakikisha kuwa wafugaji wote wanachanja kwa kuzingatia Sheria, ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wale wanaokaidi kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali;
(o) Kuandaa taarifa za zoezi la utoaji chanjo yenye takwimu sahihi na kuwasilisha Wizarani na;
(p) Kufungua mfuko wa kuendeleza mifugo ambapo fedha za kuendesha chanjo na shughuli zingine za kuendeleza mifugo zitahifadhiwa. Mfuko huu utachangiwa na 15% ya mapato yanayotokana na mifugo kama ilivyoelekezwa na Waraka wa Rais namba 1 wa mwaka 2002 wa kudhibiti magonjwa ya mifugo Tanzania.

### 7.5 Majukumu ya Watoa Huduma Binafsi

(a) Kuhakikisha kuwa wamekidhi matakwa ya kisheria na kitaaluma ya utoaji wa huduma ikiwemo za chanjo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Veterinari ya 2003 ikiwa ni pamoja na kusajiliwa na Baraza la Vaterinari;
(b) Kushiriki katika maandalizi ya awali ya chanjo yatakayoshirikisha vikao baina Halmashauri na wadau na pale inapowezekana Wizara ya Mifugo na Uvuvi;
(c) Kushirikiana na vyama vya wafugaji katika eneo husika katika uhamasishaji na ufuatiliaji wa ufanisi katika utoaji chanjo;
(d) Kutumia chanjo zilizothibitishwa ubora na kusajiliwa ama kuruhusiwa kutumika na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na Kurugenzi ya Huduma za Mifugo;
(e) Kuhakikisha kuwa chanjo zote zinatunzwa katika mnyororo baridi ili kulinda ubora wake;
(f) Makampuni yaliyopata kazi ya chanjo kuhakikisha yanafuata taratibu zote zilizowekwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mamlaka nyingine za Serikali juu ya utoaji wa chanjo za wanyama;
(g) Kuweka au kujaza aina ya chanjo, tarehe na jina la mchanjaji kwenye daftari la kumbukumbu ya chanjo la mfugaji na;
(h) Kuandaa taarifa sahihi za chanjo na kuziwasilisha kwa Daktari wa Mifugo wa Halmashauri au Wilaya husika.

### 7.6 Majukumu ya Serikali ya Kijiji au Mtaa

(a) Kuandaa kishirikishi maeneo na miundombinu ya kutolea huduma ya chanjo;
(b) Kushirikiana na vyama vya wafugaji na viongozi wa mitaa kuhamasisha umuhimu wa chanjo kwa wafugaji wote na kuhakikisha kila mfugaji anashiriki kikamilifu kwenye zoezi la chanjo;
(c) Kuhakikisha wafugaji wote wanapeleka mifugo yao kwenye vituo vya chanjo kulingana na ratiba ya chanjo;

(d) Kutunza daftari la kumbukumbu za chanjo katika mifugo yao kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Mifugo Wilaya ama Kata, Kijiji au Mtaa;
(e) Kuweka mazingira wezeshi ya kufanyika kwa utoaji huduma za chanjo na ukaguzi wa afya ya mifugo na ufanisi wa chanjo kufanyika katika maeneo yao;
(f) Kutoa taarifa kwa Afisa Mifugo wa Kata, Kijiji, Mtaa au Wilaya pale ambapo kutakuwa na madhara au athari zozote zinazodhaniwa kuwa zimetokana na chanjo na;
(g) Kutoa taarifa kwa Afisa Mifugo wa Kata, Kijiji, Mtaa au Wilaya pale inapotokea baadhi ya wafugaji kukaidi kuchanja mifugo yao na inapowezekana kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kutumia Kanuni za Chanjo na Uchanjaji za Mwaka 2020.

### 7.7 Majukumu ya mfugaji

(a) Kushiriki katika kuandaa eneo na miundombinu ya kutolea huduma ya chanjo;
(b) Kushirkiana na vyama vya wafugaji na viongozi wa Vijiji au Mitaa kuhamasisha umuhimu wa chanjo kwa wafugaji wengine katika zoezi la chanjo;
(c) Kupeleka mifugo kwenye vituo vya chanjo kulingana na ratiba ya chanjo;
(d) Kutoa taarifa kwa Afisa Mifugo wa Kata, Kijiji au Mtaa ama Uongozi wa Kijiji au Mtaa pale ambapo kutakuwa na madhara au athari zozote zinazodhaniwa kuwa zimetokana na chanjo;
(e) Kulipia gharama za chanjo kama inavyoelekezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ama uongozi wa Halmashauri kwa maeneo husika na;
(f) Kutunza daftari la kumbukumbu za chanjo zinazotolewa katika mifugo yake kwa lengo la kusadia ufuatiliaji wa kiwango cha uchanjaji, ubora na watoa huduma pale inapohitajika.

## 8. UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu wa utoaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo kwa ushirkiano katika ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi utaanza kutumika mwezi Januari, 2021. Hivyo, mdau yeyote atayeenda kinyume cha mwongozo huu katika kutekeleza majukumu ya chanjo kwa wanyama atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo.